

# WIZARA YA MALIASILI NA UTALII

## MAMLAKA YA USIMAMIZI WA WANYAMAPORI TANZANIA (TAWA)



### TAARIFA KWA UMMA

#### KUFUNGULIWA KWA UWINDAJI WA WENYEJI NA WAGENI WAKAZI NCHINI

Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) ilianzishwa mwaka 2014 chini ya kifungu cha 8 cha Sheria ya Kuhifadhi Wanyamapori Namba 5 ya mwaka 2009 likiwa ni Shirika la Umma chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii. TAWA ina jukumu la kusimamia uhifadhi wa wanyamapori na matumizi endelevu katika maeneo yaliyo nje ya Hifadhi za Taifa na Eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro.

Uwindaji wa Wenyeji na wa Wageni wakazi ni moja ya matumizi ya wanyamapori yanayosimamiwa na TAWA. Uwindaji huu ulisitishwa kwa Tangazo la Serikali Na. 538 la mwaka 2015 ili kutoa fursa ya kufanya tathmini baada ya kubaini ukiukwaji wa kanuni za uwindaji. Katika mwaka wa fedha 2017/2018 TAWA ilifanya tathmini ya uwindaji wa Wenyeji na wa Wageni wakazi nchini ili kutafuta namna bora ya kuboresha usimamizi wake.

Kufuatia tathmini hiyo, Waziri wa Maliasili na Utalii ameridhia kufunguliwa kwa uwindaji wa Wenyeji na Wageni wakazi. Aidha, Serikali imetenga vitalu vya uwindaji wa Wenyeji na wa

Wageni wakazi katika kanda tano ili kufanyiwa majaribio ya utekelezaji wa mfumo mpya wa usimamizi. Kanda hizo ni Kaskazini, Kusini, Mashariki Magharibi na Kati kama ilivyooneshwa katika jedwali:-

### Mgawanyiko wa Vitalu vya uwindaji wa wenyeji katika kanda tano

Na	Jina la Kanda	Mkoa	Kitalu cha Uwindaji	Wilaya
1	Kanda ya Kaskazini	Manyara	Kitwai Kusini	Simanjiro
2	Kanda ya Kusini	Lindi	Kilwa Kaskazini (Kilwa Open Areas North)	Kilwa
3	Kanda ya Mashariki	Pwani	Kisarawe (Kisarawe Open Areas)	Kisarawe
4	Kanda ya Magharibi	Tabora/Katavi	Ugalla Niensi (Ugalla Niensi Game Controlled Areas)	Mlele/Kaliuwa
5	Kanda ya Kati	Singida	Simbanguru/Igwemadete(Simbanguru Open Areas)	Manyoni

TAWA inapenda kuufahamisha Umma kuwa uwindaji wa Wenyeji na wa Wageni wakazi umeruhusiwa kufanyika katika vitalu vilivyotengwa kuanzia sasa. Hivyo, kwa Mtanzania yeyote mwenye nia ya kuwinda kwa ajili ya kitoweo afike kwenye ofisi za Halmashauri katika maeneo hayo au ofisi za TAWA zilizo karibu na kuwasilisha maombi ya leseni ya kuwinda.

Aidha, tunapenda kuwakumbusha wananchi wote kuzingatia Sheria, Kanuni na taratibu wakati wote wa zoezi la uwindaji wa Wenyeji na wa Wageni wakazi ikiwa ni pamoja na kuandaa nyara zote (ngozi, fuvu, n.k) zitokanazo na uwindaji wa kitoweo na kuziwasilisha kwa maafisa leseni wa TAWA.

Imetolewa na:

Mkurugenzi Mkuu,  
Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania – TAWA  
Barabara ya Dar es Salaam, Eneo la Kingolwira, Jengo la TAFORI,  
S.L.P 2658, **MOROGORO.**

Tarehe: 24 Oktoba, 2018

Kwa maelezo zaidi kuhusu uwindaji wa wenyeji na wageni wakazi tafadhali wasiliana na:

**Simu:** +255 23-293424; Barua pepe: [dq@tawa.go.tz](mailto:dq@tawa.go.tz); tovuti: [www.tawa.go.tz](http://www.tawa.go.tz)